Jinsi ya kutumia mwongozo huu

3.1	Mawanda ya mwongozo huu	17
3.2	Mtazamo wa ETI	18
3.3	Mfumo wa utekelezaji	19
3.4	Kusimamia viwango vya kazi vya wakulima wadogo na wafanyi kazi wao	21

ARDHI YA KUPANDA MAHARAGWE YA KIFARANSA, KITABU CHA PICHA, PICHA NA.4

Jinsi ya kutumia mwongozo huu

Sura hii ni muhimu kusomwa na watumiaji wote wa mwongozo huu kwa sababu inafafanua utaratibu wa utekelezaji wa mwongozo wenyewe. Inaeleza kwa muhtasari mawanda ya mwongozo huu, inapanga utaratibu wa hatua kwa hatua wa kutumia mwongozo na vilevile inaonyesha jinsi ya kunufaika zaidi kutokana na mwongozo.

3.1 Mawanda ya mwongozo

Kama ilivyoelezwa awali, mwongozo huu unalenga kukidhi mahitaji ya washiriki mbalimbali ambao wana dhima na majukumu tofautitofauti. Ili kurahisisha utumiaji wa mwongozo, tumeandika sura mojamoja kwa kila mshiriki mkuu huku tukionyesha yale ambayo wanaweza kufanya ili kuboresha viwango vya kazi. Sura zinawalenga; wauzaji rejereja **(sura ya 4)**, Wanunuzi (kundi pana la watu tofautitofauti **(sura ya 5)**, wakulima wadogo **(sura ya 7)** na mashirika yasiyo ya kiserikali **(sura ya 8)**. Tafiti mbalimbali katika matini hii zinaonyesha yale ambayo wanunuzi na vyama vya wafanya kazi wamejaribu tayari na matokeo yake.

Kundi la mradi huu limeunda mpangilio wa zana za utendaji utakaosaidia utaratibu wa utekelezaji. Kwa kuwa zana hizi zitatumika na makundi mengi, tumetoa zana za kufanya kazi kwa wote **(sehemu A hadi G)** ambazo zinatupatia:

- Mfumo wa utumiaji unaotoa viwango vyote muhimu vya kazi kutoka kwa mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI, pamoja na maana yake katika muktadha wa wakulima wadogo **(Zana za kufanyia kazi fungu A)**. Zana hizi pia zinaonyesha yale ambayo wanunuzi na wakulima wadogo au wafanya kazi wao wanaweza kufanya ili kufikia viwango vya kazi vilivyotambuliwa. Kila anayelengwa na mwongozo huu ahitajika kurejelea zana hii muhimu;
- Utangulizi wa zana ya makadirio ya mahitaji na vipaumbele, mtazamo unaopendekezwa wa kupata habari kuhusu hali za wakulima wadogo **(zana za kufanyia kazi fungu B)**. Zana hii inaweza kutumiwa na mtu ye yote anayekadiria masharti ya kazi katika mashamba madogo;
- Maswala kuhusiana na mfumo wa utumiaji ambao wanunuzi wanaweza kutumia kama kigezo cha kukadiria masharti katika mashamba madogo. **(zana za kufanyia kazi fungu C);**
- Sampuli ya barua na hojaji za wauzaji rejereja zitakazotumwa kwa wanunuzi ilikwanza kuwapanga wakulima wadogo katika mtungo wa ugavi. **(zana za kufanyia kazi fungu D);**
- Sampuli nne za nyaraka kwa wakulima wadogo na wale wanunuao moja kwa moja k utoka kwao. **(Zana za kufanyia kazi fungu E)**;
- Sampuli ya kijitabu kwa wakulima wadogo cha kuwajulisha dhana ya viwango vya kazi **(zana za kufanyia kazi fungu F)**;
- Vielelezo vya kufundishia vitakavyofafanua dhana ya mitungo ya ugavi kwa wakulima. Huu ni mfuatano wa picha, ambao fungu lake moja linaonyeshwa katika **zana za kufanyia kazi fungu G**. Kitabu kizima cha picha kinapatikana katika CD-ROM.

Masimulizi ya CD-ROM ya mwongozo huu yamo katika sehemu ya mwisho wa mwongozo. Nayo yanajumuisha mfuatano wa PDF wa **Sura ya 1 hadi 9**. Nazo **zana za kufanyia kazi** zimo katika hati za Word ili watumiaji waweze kubadili vifungukuambatana na mahitaji ya wanunuzi, wakulima wadogo na washiriki wao wengine. Kama ilivyoelezwa, CD-ROM pia ina kitabu kizima cha picha.

3.2 Mtazamo wa ETI

ETI inatambua dhima muhimu ya wakulima wadogo katika uzalishaji. Twawasishi washiriki kufanya vivyo hivyo. Hata hivyo, hatupendelei kununua kutoka kwa wakulima wadogo badala ya mashamba makubwa kama njia ya kuepuka wajibu wetu kwa wafanya kazi. Mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI (8.2) unaeleza bayana kwamba 'wajibu kwa wafanya kazi hautaepukwa kwa kutumia mkataba wa ajira pekee au mkataba mdogo wa kufanyiwa kazi peke yake'. Iwapo maendeleo yatapatikana uwajibikaji usioyumba wa kuboresha viwango vya kazi miongoni mwa wakulima wadogo ndio msingi wa kwanza na wa lazima.

3.2.1 Mtazamo wa aste aste

Mtazamo wa ETI husisitiza kupatikana maendeleo ya kiasteaste kwa viwango vya kazi katika muda uliowekwa. Mtazamo huu unafaa katika muktadha wa mkulima mdogo kama ilivyo katika ajira rasmi. Tunatambua kwamba kutimizwa kwa viwango vya mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI na wakulima wadogo kunaelekea kutokuwa rahisi au haraka iwapo kutafanywa kwa ukamilifu na uendelevu. Makampuni yanayofanya kazi na wakulima wadogo yatahitaji kuonyesha uwajibikaji wao kwa wakulima wadogo na utekelezaji wa kanuni hizo pamoja nao wakati huohuo wakidhihirisha uwajibikaji wao.

3.2.2 Kuzidi viwango vya chini kabisa

Mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI una viwango vya chini kabisa wala sio vya juu kabisa. Makampuni yanahimizwa kupita viwango vya chini kabisa. Ingawa hati hii inaeleza utendaji bora wa kutekeleza viwango vya chini kabisa, kuna vifungu vya hati hii vinavyoonyesha utendaji bora kabisa na makampuni yanahimizwa kuutekeleza kila iwezekanapo.

3.3 Mfumo wa utekelezaji

Kazi ya kundi la wakulima wadogo wa ETI imeonyesha kuwa uwajibikaji na vitendo unahitajika katika madaraja yote ya mtungo wa ugavi ili viwango vya kazi viweze kukadiriwa kwa ufanisi na kuboresha matokeo ya kazi za wakulima wadogo na wafanya kazi wao. Kwa hivyo, mfumo wa utekelezaji unaofuata unategemea vitendo vya wahusika katika madaraja yote. Mfumo huu sio mfano wa masharti yatakayofuatwa, bali unafuata mtazamo uliopendekezwa, kama inavyoonyeshwa na mchoro unaofuata.

Mfumo huu wa utekelezaji unawatambua washiriki wa daraja ya chini wa mtungo wa ugavi kuwa kiini cha mtazamo huu. Mfumo wenyewe umebuniwa haswa kulingana na uchangamano na kiwango cha wakulima wadogo. Vilevile mtazamo huu unaweza kubadilishwa kutegemea hulka za wakulima wadogo na unaonyesha nani afanye nini katika kila hatua.

Mfumo huu, kama ulivyo mwongozo wote, ni wa kijumla. Unatoa ushauri kwa wale wanaofanya kazi na wakulima wadogo, lakini utahitaji kubadilishwa ili kuambatana na bidhaa, kiwanda, nchi na mtungo wa ugavi mahsusi unaowahusu wakulima wadogo.

3.3.1 Utekelezaji wa hatua kwa hatua

Mchoro huu unaonyesha mapendekezo yetu kuhusu hatua zinazohitajika katika utaratibu wa utekelezaji. Hatua mojamoja inatekelezwa kabla ya kuingilia hatua inayofuata. Ikiwa muuzaji wa rejareja au mnunuzi hafuati kanuni za ushauri, basi kazi ya utekelezaji haiwezi kufanyika katika madaraja ya chini ya mtungo wa ugavi.


HATUA YA 1
Wanunuzi wa rejareja na wanunuzi (na mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya wafanyikazi washiriki) wanajitolea kuwajibika kwa mitazamo ya mwongozo huu.
HATUA YA 1
Wanunuzi wa rejareja na wanunuzi wanaowatafuta wakulima wadogo katika mtungo wa ugavi na kuteua kigezo cha kupimia hali za kikazi katika mashamba madogo.
HATUA YA 1
Wanunuzi au wauzaji wa rejareja (labda pamoja na vyama vya wafanyikazi na mashirikayasiyo ya kiserikali) wanakadiria wazalishaji wakitumia mfumo wa makadirio ya mahitaji na vipaumbele kama msingi wao.
HATUA YA 1
Wanunuzi au wauzaji wa rejareja wanaunda na kutekeleza mpango wa maendeleo
HATUA YA 1
Wanunuzi au wauzaji rejareja. Kuchunguzwa wa mwongozo uwe kifaa cha marejeo
'Mwongozo wa ETI kwa wakulima wadogo' kama zana ya maregeo

HATUA YA 1 KUJITOLEA KUWAJIBIKA

Kujitolea kuwajibika na matakwa ya mwongozo huu ndio hatua ya kwanza muhimu. Wauzaji warejareja na wanunuzi watahitaji kuelewa kiukamilifu viwango vya kazi tunazolenga pamoja na vitendo vinavyopendekezwa kutumika. Viwango hivyo vimeelezwa katika zana za kufanyia kazi, fungu A. Kuna ushauri zaidi kwa wauzaji wa rejareja katika **sura ya 4,** na kwa wanunuzi katika **sura 5.** Dhima za mashirika yasiyo ya keserikali na vyama vya wafanya kazi kama ilivyoelezwa katika **sura 7 na 8** pia itasaidia katika utekelezaji wa viwango vya kikazi vinavyohusika.

HATUA YA 2 KUWATAFUTA NA KUWAFAHAMU WAKULIMA WADOGO

Hatua inayofuata ni ya kuwatafuta wakulima wadogo walio katika mtungo wa ugavi pamoja na kutambua hulka zao. Hii inahusisha kutambua mahali wakulima wadogo walio kwenye mtungo waliko, na vilevile kiwango na hulka ya mtungo huo. Pia inahusisha saizi na idadi ya mashamba madogo, aina za mmea au mimea, utegemezi, muundo wa muungano, mpangilio wa kazi na kadhalika. Wanunuzi wanaweza kuteua kigezo cha kupimia hali za kikazi katika mashamba wakijitayarisha kuingia hatua inayofuata. (Angalia **zana za kufanyia kazi fungu C** kwa ushauri).

HATUA YA 3 KUKADIRIA MAHITAJI NA VIPAUMBELE VYA WAKULIMA WADOGO

Hii inahusu makadirio ya mahitaji na vipaumbele kwa wakulima wadogo. Sababu ya kimsingi ya kufanya haya inaelezwa katika **fungu la 3.4**. Matokeo ya makadirio haya yatakuwa msingi wa kiutendaji wa utekelezaji wa maendeleo katika daraja la mkulima mdogo. Mahitaji na vipaumbele vya wakulima na wafanyakazi yanaweza kulinganishwa na viwango vya mfumo wa kanuni za kimsingi za ETI kama zilivyoelezwa kwenye **zana za kufanyia kazi fungu A**. Ulinganishi huu utasababisha kupatikana kwa masuala lengwa muhimu yatakayotegemewa na wanunuzi na wauzaji wa rejareja katika kazi zao na vilevile katika kuzua maendeleo.

Baadhi ya masuala yaliyotambuliwa na wakulima wadogo/wafanyaka kazi huenda yasihusiane na masuala ya viwango vya kazi. Kwa mfano, yanaweza kuwa masuala ya usimamizi. Hata hivyo yanaweza kuwa masuala ambayo kiwanda/muuzaji wa rejareja aliye na hiari anaweza kusaidia kubadilisha kwa manufaa ya mkulima mdogo, hivyo basi kuendeleza kiwango cha usimamizi wao, na bila kukusudia, viwango vyao vya kazi.

Makadirio ya mahitaji vilevile yatawawezesha wauzaji wa rejereja na wanunuzi kutambua ni mazao ghani yanaleta faida nzuri na pia jinsi ambavyo wauzaji wa rejareja na wanunuzi wanaweza kuchangia kwa upatikanaji wa rahisi wa riziki na kanuni bora za kazi ya wakulima wadogo na wafanya kazi wao. Haya yatatupatia picha bayana ya uendeshaji wa ukulima mdogo, na kuwafanya wanunuzi, wauzaji wa rejareja, mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya wafanya kazi kutambua sehemu muhimu za kazi ya wakulima wadogo ambazo hazipaswi kuwachiliwa kuadhirika vibaya.

HATUA YA 4 KUUNDA NA KUTEKELEZA MPANGO WA MAENDELEO

Ni muhimu kukiri kwamba aina tofautitofauti za wakulima wadogo, pamoja na sekta ya kilimo isiyo rasmi inasababisha ugumu wa kuchagua na kutumia mtazamo mmoja wa maendeleo. Mtazamo unaoweza kubadilishwa kama inavyotakiwa ndio unaonekana kuwa njia bora zaidi ya kufanikisha lengo hili. Jinsi na aina za maendeleo yatakayotekelezwa yatategemea matokeo ya makadirio ya mahitaji, hali za urasmi wa uhusiano wa kikazi na chaguo la mtazamo utakaofaa zaidi mtungo wa ugavi na bidhaa mahsusi. Makampuni mengine huenda yakatoa mafunzo kwa wagawaji na wakulima wadogo/wafanya kazi, au kuchukua mtazamo usio dhahiri kwa kufanya urekebishaji wa kiunzi cha shirika lao ili wajiendeleze wenyewe. Aidha, baadhi ya makampuni yatajitolea kufanya ukaguzi wa mahesabu na, wengine sampuli za ukaguzi wa mahesabu. Ingawa mchanganyiko wa baadhi ya mitazamo hii unaweza kuwafaa, uamuzi sharti ukague moja moja ya kila hali zilizopo.

Hali za wakulima wadogo zilizo dogo na rasmi zaidi, ndizo zinazofanikisha zaidi upatikanaji wa viwango vya juu vya kazi. Katika sekta isiyo rasmi, wanunuzi wanahitaji ushirikiano na imani ya wakulima zaidi kuliko katika sekta iliyo rasmi. Ushirikiano, kwa vyovyote vile, hauwezi kulazimishwa.

Kwa mfano, pale ambapo wanunuzi wana kiasi fulani cha madaraka ya kiuchumi, mtungo wa ugavi ulio nusu-rasmi na idadi ya wakulima inayoweza kusimamiwa, ule mtazamo wa kutoka juu kwenda chini unaweza kuleta mabadiliko kadha. Katika hali hii, wanunuzi au wauzaji wa rejereja huenda wakatumia ukaguzi wa mahesabu na ununuzi mchache zaidi unaohitajiwa na wakulima. Ili kupata matokeo yanayotarajiwa, muundo wa ukaguzi huo unapaswa kuhusisha masuala yaliyotambuliwa katika makadirio ya mahitaji. Vilevile ukaguzi huo unapaswa kuzingatia kwa uangalifu masuala muhimu zaidi kwa wakulima wadogo wadogo na wafanya kazi wao. Hata hivyo, pale ambapo kuna idadi kubwa zaidi ya wakulima wadogo na ukosefu mkubwa wa usimaizi, nguvu za kiuchumi za kiwango cha chini kabisa, pamoja na ukosefu wa uwezo wa wakulima, mtazamo utakaoleta ufanisi ni ule unaoegemea zaidi kunako mahitaji na vipaumbele. Katika hali hii, ununuzi kutoka kwa wakulima utaleta matatizo; hivyo basi, mtazamo wa mahitaji na vipaumbele ulio mpana utahitajika ulenge masuala ambayo wakulima wadogo/wafanya kazi wametambua wenyewe.

Kuchukua hatua: Kutumia mfumo wa utekelezaji kama zana ya marejeo.
Mara tu ukadiriaji umeshafanywa, mfumo wa utekelezaji **(zana za kufanyia kazi fungu A)** unapaswa kutumiwa kama zana ya marejeo. Hii inatoa ushauri usio na utata kuhusu hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa na wanunuzi katika kushughulikia hali za kikazi za wakulima wadogo na wafanya kazi wao chini ya kila sehemu ya mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI, pamoja na viashirio ili kupima ufanisi wa hatua hizo.

Miundo ya wakulima wadogo
Ni muhimu kuzingatia miundo ya mtungo wa ugavi wakati tunapanga maendeleo. Mbinu za ushirikiano katika muungano wo wote wa wakulima wadogo hupitia miundo ya wahisika wenyewe. Miundo hii inaweza kuwa kundi lililochaguliwa katika kiwango cha mtaa au mkoa kama vile chama cha ushirika au miundo kama vile vituo vya kukusanya/ kununua bidhaa katika jamii. Miundo hii itakuwa imetambuliwa kwenye shughuli za kutathmini makadirio ya mahitaji. Vilevile ni muhimu kuwajumuisha na kuwahusisha katika kupata mashauri wanachama wa vikundi vya wakulima na wafanya kazi hasa kuhusu jinsi ya kutekeleza mabadiliko.

HATUA YA 5 KUFUATILIA
Shughuli yoyote iliyotekelezwa na wakulima wadogo inapaswa kutathminiwa kila baada ya kipindi fulani, iwe ni ile ya ukaguzi wa mahesabu, mafunzo yaliyotolewa au mabadiliko ya kiusimamizi. Ni muhimu kuchambua mitazamo ya mipango na utekelezaji, ukibadili utekelezaji kila inapobidi. Tathmini za kila baada ya kipindi fulani zinahitaji zifanywe katika kiwango cha mitaa na zijumuishe majibu kutoka wakulima wadogo na wengineo walio katika mtungo wa ugavi.

3.4 Kusimamia viwango vya kazi vya wakulima wadogo na wafanya kazi wao

Kanuni kuu ya mwongozo ya kundi la ETI inazingatia kwamba kazi yo yote iliyofanywa ili kuhakikisha kuwa hali za kikazi za wakulima wadogo na wafanya kazi zinadumisha viwango vya mifumo ya kimsingi ya kanuni, haipaswi kuwabagua wala kuudhoofisha uwezo wao wa kutimiza viwango hivyo. Uzoefu wetu wa kutumia njia mbalimbali za kusimamia na kukadiria viwango hupendelea matumizi ya makadirio ya mahitaji na vipaumbele kuliko ukaguzi wa mahesabu wa kawaida. Sehemu zifuatazo zinaonyesha yaliyopelekea kuzindua uamuzi huu.

3.4.1 Je, ukaguzi wa kazi unafaa kwa wakulima wadogo?

Njia ya kawaida inayotumiwa na wauzaji wa rejereja na wanunuzi kukadiria viwango vya kazi ni ile ya ukaguzi (wa mahesabu) wa kukadiria wakulima katika muktadha wa viwango vya mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI. Tajriba yetu inaonyesha kuwa ukaguzi sio zana ifaayo kutathminia mafanikio ya wakulima wadogo pamoja na wafanya kazi wao hasa iwapo madhumuni ni kupata picha halisi ya hali na kanuni zao za kikazi. Jambo hili linaakisi matatizo mengi kama yale yatokanayo na matumizi ya ukaguzi wa mahesabu katika mazingara rasmi ya kazi kama vile mashamba makubwa au viwanda. Ukaguzi wa kawaida huenda ukatoa habari zenye manufaa lakini waweza kushindwa kutoa habari za jinsi ya kuleta maendeleo ya kudumu kwa wakulima wadogo na wafanya kazi bila ya kuwadhuru katika utaratibu huo. Ukaguzi wa kawaida wa kazi:

- Unajumuisha sio tu ushahidi wa matamshi bali pia ule ulinganishaji wa marejeo ya kumbukumbu na miundo ili kusaidia shughuli za lazima za kufanya kazi hiyo. Ulazimu wa kuweka kumbukumbu na miundo iliyoandikwa katika kipindi cha muda mfupi huenda usiwezekane kati ya wakulima wadogo ambao hawahusiani moja kwa moja na muuzaji wa soko la nje ila hilo liwe sharti la kuthibitisha utiifu kati ya wanunuzi wa nchi za nje;
- Unahitaji mkulima kuthibitisha kiwango fulani cha utiifu badala ya mkaguzi wa mahesabu kuthibitisha ukosefu wa utiifu.

Mtazamo huu:

- Hauiani vyema katika muktatha usiowajibisha mkulima mdogo kuzingatia mifumo rasmi na dhana ya kuthibitisha utiifu. Kwa kweli, pale ambapo mifumo rasmi imetekelezwa kuedndeleza ukaguzi wa utiifu, pamezuka matatizo;
- Ni finyu, ukiwapa wagawaji na wauzaji wa rejareja taswira ya yale yanayotokea wakati wa ukaguzi ikilinganishwa na kanuni za kazi. Ukaguzi hautuelezi kuhusu muktadha mpana wa hali lengwa au jinsi bora za kuleta maendeleo ya kudumu;
- Hauelezi kikamilifu mahitaji au masuala yaliyo muhimu kwa wakulima wadogo na wafanya kazi wao. Ikiwa wauzaji wa rejareja na wagawaji wananuia kuinua viwango vya kazi, basi kuelewa kwa upana mazingira wanamofanyia kazi wakulima wadogo na wafanya kazi wao ni jambo la lazima.

3.4.2 Gharama ya ukaguzi wa viwango

Ipo idadi kuwa ya wakulima wadogo wa aina mbalimbali ambao mara kwa mara huwa wamesambaa katika eneo kubwa kijiografia. Kwa wingi wao hutegemea miundo tofautitofauti ya mitungo ya ugavi, kama vile vyama vya ushirika, uhusiano wa moja kwa moja na wauzaji bidhaa kwenye soko la nje au kupitia uajenti unaomilikiwa na serikali. Kwa hivyo, mfumo wowote wa ukaguzi wa kazi kwa wakulima wadogo, iwe ni ukaguzi wa watu wote au hata sampuli ya ukaguzi, huweza kugharimu sana na pia kutumia muda mwingi. Gharama ya kufanya ukaguzi huenda ikawaumiza wakulima wadogo. Je, kwa nini wagawaji wafanye ukaguzi mahali kadha wa kadha badala ya kufanya hivyo kwenye shamba kubwa moja ambapo kazi itakuwa chache na gharama iwe chini? Kusisitiza kufanywa ukaguzi kutahimiza kutengwa kwa, sio tu mzalishaji mdogo, bali pia vibarua wao ili iwanufaishe wazalishaji wakubwa. Matokeo yake ni kuhatarisha utolewaji wa bidhaa za hali ya juu ambazo baadhi ya wakulima wadogo wana uwezo wa kuzalisha.

3.4.3 Uhusiano baina ya 'kazi ya ushirika' na riziki za wakulima wadogo/wafanya kazi

Unapofanya kazi na vikundi vinavyoweza kudhulumiwa, kama vile wakulima wadogo na wafanya kazi wao, nafasi ya kufanya makosa huwa ndogo. Kazi za wakulima wadogo na wafanya kazi huenda zikawa mashakani kutokana na matokeo yasiyotarajiwa ya kazi yo yote ya ushirika. Vilevile, hili litadhoofisha zaidi uwezo wao wa kunufaika na uhusika wao katika mtungo wa ugavi, au hata kuwaondoa kabisa kutoka mtungo. Wagawaji, na hasa wauzaji wa rejareja na wateja wanunuao kutoka kwao, wanahitaji kufahamu vyema hali za wakulima wadogo na miktadha yao ya kikazi. Mfumo wa ukaguzi wa kijumla /ukaguzi wa mahesabu wa kawaida hautoi nafasi ya kupanua ufahamu huu.

3.4.4 Uwezo wa wakulima wadogo wa kutekeleza mabadiliko

Pale ambapo ukaguzi wa kijumla au ukaguzi wa mahesabu unagundua masuala yatakiwayo kutatuliwa miongoni mwa waajiri rasmi, ni juu ya kampuni iliyokaguliwa kutekeleza mabadiliko ili kutimiza viwango vya kazi vinavyotakiwa. Hata hivyo, tajriba yetu inaonyesha kuwa wakulima wadogo hawawezi kutarajiwa 'kutimiza' viwango fulani vinavyofuata utaratibu rasmi wa ukaguzi. Yamkini kusiwe na uwezekano wa kuwa na muundo wo wote wenye kufafanua utaratibu huo ifaavyo au wenye kujenga uwezo wao wa kutimiza viwango. Zaidi ya hayo, huenda wasione matakwa haya kuwa ya manufaa yo yote kwa wakulima wadogo au wafanya kazi wao. Aghalabu, wakulima wadogo huwa mwishoni mwa mtungo wa ugavi, na mara nyingi bila ujuzi, uwezo au nguvu za kupata usaidizi wa kutimiza viwango.

3.4.5 Mtazamo wa makadirio ya mahitaji

Tunapendekeza kuzingatia mtazamo wa makadirio ya mahitaji na vipaumbmele kama kibadala cha ukaguzi wa kijumla /ukaguzi wa mahesabu wa viwango. Kundi lilishauriana na wagawaji wa wanachama, wenzi wao na washiriki (pamoja na maafisa wa serikali) wote wakiwa wanafanya kazi katika sekta ya chai na mazao mabichi nchini Kenya mnamo Oktoba 2003. Wale walioulizwa maswali walipendekeza kufanywe makadirio ya mahitaji pamoja na wakulima wadogo ili kupata ufahamu wa hakika wa hali, mahitaji na vipaumbele vya wakulima wadogo na wafanya kazi wao. Utumiaji methodolojia ya utafiti ulioshirikishwa kazi hii ulileta habari za hali ya juu. Kutokana na hayo, methodolojia hiyo ya utafiti imerekebishwa ili itumiwe na wale wanaotaka kuitumia kama kifaa cha kukusanya habari na cha kukadiria muktadha mpana na viwango vya kazi vya wakulima na wafanya kazi wao. Mtazamo huu huenda ukahitaji matayarisho zaidi na ni lazima utumiwe kwa kufuata methodolojia iliyopendekezwa. Hata hivyo, mtazamo huu unaweza kutumiwa kwa hali za wakulima wadogo na haugharimu sana. Mtazamo huu umeelezwa katika **zana za kufanyia kazi, fungu B.**

Tunapendekeza kwamba wasomaji wote sasa waangalie mfumo wa utekelezaji katika **zana za kufanyia kazi fungu A** kabla ya kuingilia sura zilizoandikiwa kila kundi.